# Ng'ombe waliovushwa kwa magendo nchi jirani wakamatwa

NA SAMSON CHACHA, *TARIME*

MAOFISA mifugo Wilaya ya Tarime, wanavijiji vya Remagwe, Ubiterere, Ng'ereng'ere na Kitagasebe wamekamata ng'ombe 118 wanaosadikiwa kuvushwa kimagendo kwenda nchi jirani.

Akizungumza wiki iliyopita katika mnada wa mifugo wa Magena, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mntenjile, alitoa onyo kwa wafanyabiashara wa magendo ya mifugo kuacha mara moja vitendo hivyo.

Alisema ng'ombe hao 118 walisafirishwa bila vibali kwa lengo la kupelekwa nchi jirani kupitia njia za panya ambapo wananchi kwa kushirikiana na maofisa wa serikali walifanikiwa kuzuia tukio hilo.

"Wafanyabiashara wa mifugo mnatakiwa kufanyabiashara za mifugo kwa kufuata taratibu na sheria za nchi, hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wafanyabiashara wanaokwepa kupitisha mifugo yao katika mnada wa Magena kwa lengo la kupeleka nchi jirani.

"Viongozi wa vitongoji, vijiji na kata mnapaswa kushirikiana na kushirikiana na vikundi shirikishi na askari wa akiba waliopo katika maeneo yao kudhibiti biashara haramu ya magendo mipakani," alieleza.

Alisema serikali haizuii wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kuja kununua mifugo nchini na Tanzania, hawazuii kusafirisha mifugo kwenda nchi jirani, bali wanapaswa kufuata taratibu zilizopo.

Naye, ofisa kutoka Wizara ya Mifugo na ambaye ndiye msimamizi wa Mnada wa Magena, Hema Mughenyi, alisema serikali inawahimiza wafanyabiashara wa mifugo kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Alisema kuna baadhi ya wenyeviti wa vijiji vya mipakani wamekuwa wakituhumiwa na wafanyabiashara wa mifugo kuandikiwa barua kuwa wananunua mifugo kwa ajili ya kilimo kumbe wananunua kwa ajili ya biashara.

Mughenyi alivitaja vijiji vinavyotumika kupenyeza mifugo kwenda nchi jirani kinyemelea ni Kubiterere, Ikoma, Kogaja, Ngerengere, Nyabisaga, Borega na Itiryo.



Scanned with CamScanner

# Upotevu dagaa Ziwa Tanganyika tishio

**Na BARAKA LOSHILAA**

KIWANGO cha upotevu wa dagaa, lumbu na mgebuka katika Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma kwa wafanyabiasahara wadogo wakati wa utunzaji, ni mkubwa, imeelezwa.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO), katika warsha ya uthibitisho wa utafiti wa mnyororo wa thamani kupitia mradi wa FISH4ACP wanaousimamia mkoani hapo, inaonyesha upotevu wa mazao hayo ni unatokea kwa asilimia 70.

Mtaalamu wa Uvuvi kutoka FAO, Hasim Muumin alisema upotevu huo unachangiwa na uvuvi, uchakataji na utunzaji usiofaa.

"Pia upotevu ni mkubwa kwa wauzaji wa jumla nje ya nchi wakati wa usafirishaji, kulinganisha na sehemu nyingine ya mnyororo wa thamani," alisema.

Hashim alisema sekta ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma, inachangia kipato kwa wavuvi 27,000 na wachakataji 11,000.

Alisema FAO kupitia utekelezaji wa mradi wa FISH4ACP ambao unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), kwa miaka mitano ukishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mashirikiano ya Uchumi ya Ujerumani.

Kupitia mradi huo, fursa za uvuvi zitafunguliwa Ziwa Tanganyika kwa kuondolewa changamoto zinazoikabili sekta ya hiyo.

Hashim alisema kupitia mradi wa FISH4ACP, watahakikisha njia bora za uvuvi, uchakataji na uhifadhi zinatumika, ili kuongeza thamani ya mazao hayo katika mnyororo wa thamani.

"Pia kukabiliana na athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya moshi katika usindikaj, tutahamasisha njia salama katika usindikaji wa samaki," alisema.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Wavuvi Tanzania, Francis John, katika kuunga mkono matokeo ya utafiti huo wa mnyororo wa thamani, alisema sekta ya uvuvi wanakabiliwa na changamoto nyingi.

"Upotevu wa samaki nyakati za mvua ni kubwa wengine wanaoza, mbali na hilo upatikanaji wa leseni ni changamoto, unapokata ya uvuvi mwezi Agosti huisha Desemba na unatakiwa kukata nyingine. Tunaomba muda wa kwisha kwa leseni uwe mwaka mmoja na siyo vinginevyo.

"Changamoto nyingine ni leseni ya chombo kuchanganywa na leseni ya mvuvi, hii inamuumiza mwenye chombo.

"Mvuvi anapoamua kuachana na mwajiri wake lazima mwenye chombo akakate leseni nyingine, tunachoona hakuna haja ya kuwa na leseni kwa mvuvi, ibaki leseni ya chombo tu, sasa mvuvi akikukimbia ukaendelea kutumia leseni uliyonayo unapigwa faini ya sh. 500,000. Hilo linatuumiza," alisema.

**DAGAA**

**UPOTEVU**

Utafiti wa mnyororo wa thamani unaonyesha sekta ya uvuvi inakabiliwa na changamoto nyingi

Scanned with CamScanner

# Jipangeni soko la nyama Saudi Arabia

hicho kusitishwa miaka 19 iliyopita, kuna taratibu zilipaswa kufanyika ili kuhakikisha huduma hiyo inarejea na zaidi katika kufanikisha hilo timu ya wakaguzi kutoka Saudi Arabia ilifika nchini Agosti Mosi mwaka huu kukamilisha taratibu zake na kutembelea Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Naipongeza serikali kwa hatua nzuri iliyoifikia ambayo ni dhahiri mbali na kuliwezesha taifa kuingiza fedha za kigeni, pia itawasaidia wafanyabiashara na wafugaji kunufaika kutokana na kuongezeka kwa soko la mifugo hivyo kuzidi kubadilisha maisha yao na familia zao kutokana na kurejea kwa fursa hiyo adhimu.

Tanzania inatajwa kushika nafasi ya pili kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo katika Bara la Afrika ikitanguliwa na Ethiopia na hivyo kuipa fursa ya kufanya vizuri katika biashara ya nyama za mifugo hiyo kulingana na matakwa ya taifa hilo na mengineyo yanayohitaji kufanya biashara ya namna hiyo na Tanzania.

Kikubwa ni wafanyabiashara wenyewe kujipanga vizuri.

Kwa kipindi kirefu Tanzania imekuwa ikisifika kwa kufanya vizuri katika biashara ya usafirishaji wa nyama za mifugo katika mataifa mbalimbali kutokana na ubora wa mifugo yake na uhakika wa upatikanaji wa nyama, huku ikiwa na mifugo ya kutosha ikilinganishwa na mataifa mengine barani Afrika.

Akizungumza na baadhi ya wafugaji nchini, Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewataka wafugaji kuhakikisha wanatumia fursa ya uwapo wa masoko ya nyama kimataifa kwa kuiongezea ubora mifugo yao ili iweze kukidhi matakwa ya soko hilo na hivyo kujihakikishia soko la uhakika la uuzaji wa mifugo yao.

Ulega amewataka wafugaji kuitumia ipasavyo fursa hiyo kwa kuinenepesha mifugo huku akiwahakikishia uwapo wa wa fedha za mikopo za uhakika kutoka Benki ya Kilimo kwa ajili ya kufanikisha jambo hilo na mengine huku akisisitiza lengo la hatua hiyo ya serikali ni kuhakikisha wananufahika na ufugaji wanaoufanya.

Nimalizie kwa kuwambukusha Watanzania kuwa Tanzania itajengwa na wao wenyewe, kikubwa zinapojitokeza fursa mbalimbali zikiwamo za kibiashara kwa bidhaa zetu tulizonazo ni vyema tukahakikisha tunazitumia ipasavyo ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi ya taifa letu na watu wake.

MSAMIATI WA LEO

HabariLEO

Mtadaruki

Scanned with CamScanner